ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001 : 2015 Certified

HALIUZWI

# Newsletter

JULAI 2023

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 36

# WANAORIDHIKA NA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA EWURA WAFIKIA ASILIMIA 80.4




**Kauli Mbiu:** *"Udhibiti wa Haki kwa Matokeo CHANYA - IMPACT"*

## Toleo Lililopita




## BODI YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. James Andilile

**MHARIRI**
Bw. Titus M. Kaguo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Bw. Wilfred Mwakalosi

**WAANDISHI**
Bi. Asiatu Msuya
Bi. Tobietha Makafu

**MAKAO MAKUU YA EWURA,**
Jengo la EWURA,
3 Mtaa wa EWURA,
41104 Tambukareli,
S.L.P. 2857, Dodoma,
Simu: +255 26 2329002-4,
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua pepe: info@ewura.go.tz;
Tovuti https://www.ewura.go.tz
Simu ya BURE 0800110030

**Mitandao ya Kijamii**
: ewuratanzania
: ewuratanzania
: ewura_tz
EWURA TV

# YALIYOMO

Kutoka kwa Mhariri ............ 3
Wanaoridhika na huduma zinazotolewa na EWURA wafikia asilimia 80.4............ 4
Wenye viwanda waagizwa kutumia mafundi umeme wenye leseni............ 5
JK afurahishwa na udhibiti wa EWURA sekta ya maji.......... 6
Prof. Mwandosya awahakikishia ushirikiano watoa huduma ...7
Dkt. Andilile: Tumieni vilainishi vilivyosajiliwa na EWURA .... 8
Fuateni sheria, wadau wa magari ya kutumia gesi asilia waambiwa ............ 9
Anachotakiwa muombaji leseni za mafundi umeme nchini sasa ni simu ya Kiganjani ............ 10
Kujisajili Kanzidata ya EWURA ni ndani ya saa 24 ............ 11
Wananchi wahamasishwa kuvuna maji ya mvua ............ 12
Iringa WSSA yawa kinara kwa ubora wa utoaji wa huduma ..... 13
EWURA kuwasaidia wazalishaji wadogo wa umeme nchini ............ 14




## PICHA YA MBELE:

*Ofisi ya EWURA Makuu Dodoma: Watumiaji wanaoridhishwa na huduma zinazodhibitiwa na EWURA wafikia 80.4% kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa hivi karibuni.*

# KUTOKA KWA MHARIRI



**Titus M. Kaguo**

**Wapenzi Wasomaji wetu!**

Ninawakaribisha wote kujiunga nasi katika toleo jipya la Jarida la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), toleo la 36 katika mfululizo wa machapisho ya Majarida ya EWURA kwa mwaka 2023.

Kwa heshima na taadhima napenda kukualika kusoma makala za kuvutia kutoka katika shughuli mbalimbali za udhibit zilizotekelezwa na EWURA. EWURA inadhibiti sekta ndogo tatu za nishati ambazo ni Petroli; Umeme na Gesi Asilia na Sekta moja ya Maji; Maji na Usafi wa Mazingira. Habari zilizoandikwa katika Toleo hili zinahusisha shughuli zilizofanyika katika kipindi cha Machi 2023 na Juni 2023 na linatoka wakati EWURA ikiwa inashiriki kikamilifu katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) kama sehemu ya utoaji wa elimu kwa umma katika kutekeleza kipengele cha 6(e) cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania.

Kipengele cha 6(e) kinasema kwamba ni wajibu wa Mamlaka kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na; haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; Njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za mamlaka kwa ujumla.

Katika Toleo hili pamoja na mambo mengine, habari zilizochapishwa ni pamoja na Watumiaji wa huduma zinazozidhibitiwa na EWURA kuridhika kwa asilimia 80.4 ya utendaji wa EWURA, Jk alivyoridhika na udhibiti wa EWURA katika Sekta ya Maji, Agizo la wadau wa Gesi Asili kufuata Sheria na habari nyingine kemkem.

***Karibuni***

# Wanaoridhika na huduma zinazotolewa na EWURA wafikia asilimia 80.4

**Na Asiatu Msuya**

Utafiti wa hivi karibuni umebaini kuwa, asilimia 80.4 ya watumiaji wa huduma wamerithishwa na huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) wakati asilimia 84.8 wakirithika na jinsi EWURA inavyotoa elimu kuhusu majukumu na utendaji kazi wake huku asilimia 69.1 ya wateja wanaotumia huduma zinazodhibitiwa wamefurahishwa na uwazi na uwajibikaji wa hali ya juu.



Akizungumzia utafiti huo, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Bw. Titus Kaguo alisisitiza kuwa, mwaka 2019, kiwango cha kurithika kwa wateja wa EWURA kilikuwa asilimia 50.0 hivyo, jitihada za dhati zilizofanyika katika kutoa elimu na uhamasishaji endelevu kwa wadau muhimu wakiwemo watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa, kuhusu utekelezaji wa shughuli zinazodhibitiwa, ndiyo zimekuwa nguzo muhimu katika mafanikio ya EWURA.

Kifungu cha 6 (e) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 kinaitaka Mamlaka kukazia kutoa elimu, taarifa na kuimarisha uelewa wa umma kuhusu sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa walaji na watoa huduma zinazodhibitiwa; njia za kuwasilisha na kutatua malalamiko na migogoro; na majukumu, kazi na shughuli za Mamlaka.

"Tunafurahi kwamba, jitihada zetu zinazaa matunda kwani utafiti umebaini kuwa asilimia asilimia 84.8 wameridhishwa na jinsi EWURA inavyotoa elimu kuhusu majukumu na utendaji kazi wake huku asilimia 73 ya wadau wetu wanafahamu jukumu la EWURA na asilimia 74.0 wamerithia kuwa Mamlaka hupokea maoni kabla ya kufanya mabadiliko yoyote kwenye huduma inazozisimamia, kwetu ni hatua kubwa". Alithibitisha Bw. Kaguo.




*Ofisi ya EWURA Makuu Dodoma: Watumiaji wanaoridhishwa na huduma zinazodhibitiwa na EWURA wafikia 80.4% kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa hivi karibuni.*

Bw. Kaguo alifafanua zaidi kuwa, matumizi ya njia mbalimbali za mawasiliano kutoa elimu na taarifa za shughuli za EWURA ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kupanga bei, haki na wajibu wa mteja, taratibu za maombi ya leseni, pamoja na uelewa kwa ujumla juu ya udhibiti, kumeimarisha ushirikishwaji wa wadau kwa mizania na katika ngazi mbalimbali.

Utafiti huo wa kubainisha hali ya kuridhika kwa wateja ulilenga kupata taarifa za kiwango cha kuridhidhishwa kwa wateja wa huduma za udhibiti zinazotolewa na Mamlaka na hali ya ufahamu wa majukumu na kazi za Mamlaka.

# Wenye viwanda waagizwa kutumia mafundi umeme wenye leseni

**Na Mwandishi Wetu**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetoa agizo kwa wamiliki na waendeshaji wa viwanda vyote nchini, kutumia mafundi umeme wenye leseni za EWURA, kufanya kazi za umeme katika viwanda vyao na kwamba ukiukwaji wa takwa hilo ni kosa linaloadhibiwa kisheria.

Katika agizo hilo, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile, kwenda kwa wamiliki wa viwanda vyote nchini amesema ni matakwa kisheria kuhakikisha mafundi umeme wote wanaofanya kazi viwandani mwao wanakuwa na leseni kabla ya tarehe 31/07/2023.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1)(a) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 na Kifungu cha 4(1) cha Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme, Tangazo la Serikali Na.287 la mwaka 2019, kwa pamoja zinamtaka mtu yeyote anayezalisha umeme kwa matumizi binafsi kwa kiasi kinachozidi MegaWati moja (1MW) kuwa na leseni inayotolewa na EWURA.

Pia Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1)(h) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 na Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji wa Mifumo ya Umeme) za mwaka 2022, Kanuni ya 4 (1) kwa pamoja zinamtaka mtu yeyote anayefanya shughuli za ufungaji wa mifumo ya umeme Tanzania Bara kuwa na leseni ya umeme iliyotolewa na EWURA.

Aidha, Dkt. Andilile aliagiza maombi ya leseni kufanywa kwa njia ya kielektoniki kupitia mfumo wa LOIS unaopatikana katika tovuti ya www.ewura.go.tz, hivyo muombaji ana uwezo wa kuwasilisha maombi yake popote alipo.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Bw. Titus Kaguo (wapili kulia), alipotembelea Banda la EWURA katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Nyeyere jijin Dar es Salaam. Kulia ni Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa EWURA, Bi Asiatu Msuya na Ofisa Uhusiano, Bi. Tobietha Makafu (Kushoto).*

Muombaji anapaswa kuambatisha nyaraka zifuatazo: nakala ya vyeti vya elimu ya ufundi umeme, wasifu wa muombaji, picha ya pasipoti ya muombaji yenye kivuli cha bluu, kitambulisho cha taifa au leseni ya udereva au hati ya kupigia kura.

Gharama za leseni zinategemea na daraja la leseni ya fundi umeme alilopatiwa, ambapo A, B, S1 na S2 ni shilingi 130,000/- na kwa daraja C, D, W na S3 ni shilingi 50,000/-, madaraja haya yamepangwa kutegemea na kiwango cha elimu cha muombaji na uzoefu wake katika kufanya kazi zau meme.

Yeyote atakayefanya kazi za ufundi umeme kinyume na sheria hii, atalipa fine ya shilingi 300,000/-, na yule atakayefanya kazi nje ya mipaka ya leseni yake akijulikana atalipa faini ya shilingi 200,000/-.

# JK afurahishwa na udhibiti wa EWURA sekta ya maji

**Na Mwandishi Wetu**

Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete aliyejulikana wakati wa utawala wake kama JK, ametembelea Makao Makuu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), wakati wa mkutano na Wizara ya Maji juu ya Programu ya Kitaifa ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji ya mwaka 2024-2030.




*Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (katikati) akiwa katika picha iliyopigwa katika ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kabla ya kushiriki mkutano na Waziri wa Maji, Mhe.Jumaa Aweso (wapili kulia). Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mabonde, Mha. Mbogo Futakamba (kushoto), Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mha. Nadhifa Kemikimba na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile (kulia).*

Akiwa EWURA, JK pamoja na masuala mengine, alipata fursa ya kuzungumza na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile, kuhusu namna Mamlaka inavyodhibiti Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira na kusisitiza kuwa ubora wa maji na huduma umeimarika kutokana na ufuatiliaji unaofanywa na EWURA ambapo aliridhika na hatua zinazochukuliwa kudhibiti Sekta ya Maji.

Akizungumzia Programu hiyo, JK alieleza kuwa, upatikanaji wa maji safi na salama imeendeelea kuwa changamoto kubwa kwa nchi za kiafrika hasa kutokana na ukosefu wa fedha za kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya maji. Alisisitiza kuwa ni lazima kila nchi kutengeneza mkakati thabiti wa kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa kila mwananchi ili angalau yafike umbali wa mita 400 kutoka kwenye makazi, kama ilivyoainishwa kwenye sera ya maji na kusisitiza kuwa jambo hilo litasaidia kuimarisha usafi wa mazingira.

JK alishiriki mkutano huo kwa kuzingatia nafasi aliyonayo ya Uenyekiti wenza wa ngazi ya juu wa Programu ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji barani Afrika (African Water Investment Programme), ambayo pamoja na mambo mengine, hujadili mikakati ya namna ya kuimarisha huduma ya majisafi, salama na usafi wa mazingira kwa nchi za Afrika. JK pia, ni Mwenyekiti wa ushirikiano wa kimataifa wa maji (global water partnership); eneo la Kusini mwa Afrika.

# Mwandosya awahakikishia ushirikiano watoa huduma

**Na Asiatu Msuya**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya, ameahidi kuwa, EWURA itaendelea kushirikiana na wadau wake wakiwemo watoa huduma zinazodhibitiwa ili kuendelea kuimarisha ushirikiano na kuhakikisha utoaji endelevu wa huduma zinazokidhi ubora na viwango.

Prof. Mwandosya alisema hayo kwa nyakati tofauti, alipokutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa wafanyabiashara wa mafuta, wazalishaji wa umeme, bodi za Mamlaka za maji na Usafi wa Mazingira, viongozi wa serikali, wizara, mashirika na wadau wengine mbalimbali ambapo alisema dhima ya Bodi ya EWURA ni kuhakikisha Mamlaka inatoa huduma ya kiwango cha kimataifa kwenye udhibiti wa sekta za nishati na maji.

"Bodi yetu itaendelea kutoa ushirikiano kwenu na kuhakikisha changamoto zilizopo zinafanyiwa kazi kwa uthabiti ili kuwawezesha kutoa huduma endelevu, niwasihi, muendelee kufuata miongozo inayotolewa na zaidi karibuni tuzungumze, milango ipo wazi," alieleza Prof. Mwandosya.

Alisema Bodi yake ina wajibu kwa mujibu wa Sheria, kuhakikisha utendaji wa Mamlaka unachagiza maendeleo katika jamii kwa kuhamasisha ushindani na ufanisi wa kiuchumi, kulinda maslahi ya watumiaji huduma zinazodhibitiwa na mitaji ya wawekezaji pamoja na upatikanaji wa huduma wa uhakika.




*Msajili wa Hazina, Bw. Nehemiah Mchechu (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile, alipotembelea EWURA hivi karibuni kwa shughuli za kiofisi .*

# Dkt. Andilile: Tumieni vilainishi vilivyosajiliwa na EWURA

**Na Asiatu Msuya**

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Dkt. James Andilile, amewataka Watanzania kutumia vilainishi vilivyosajiliwa na EWURA kwa kuwa uhalali na ubora wake umethibitishwa hivyo kutokuwa na madhara kwenye mifumo ya magari au mashine mbalimbali zinazotumia bidhaa hizo.

Mkurugenzi mkuu huyo pia ameagiza kuwa hairuhusiwi, kwa yeyote vile, kusambaza ama kuuza vilainishi vilivyojazwa kiholela katika vifungashio visivyoruhusiwa kama vile chupa za maji ya kunywa, kwa kuwa havikidhi viwango vya ubora.

Zaidi, amewaasa wafanyabiashara ya vilainishi kuzingatia kanuni inayoratibu shughuli za vilainishi ya mwaka 2022, iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 115; inayomtaka mtu yeyote kutoagiza, kutengeneza, kusafirisha, kusambaza, kuhifadhi wala kuuza vilainishi visivyosajiliwa na EWURA na kwamba atakayebainika kukiuka maelekezo hayo atakuwa ametenda kosa na atapaswa kulipa faini ya shilingi milioni 20.

“Watumiaji wa vilainishi mnunue vile vilivyosajiliwa na EWURA tu, na muepuke vilainishi vilivyowekwa kwenye chupa zisizokidhi ubora”. Alisisitiza Dkt. Andille katika tangazo lake kwa umma.

Mkurugenzi wa Petroli EWURA, Bw. Gerald Maganga, naye alieleza kuwa, EWURA itaendelea kufuatilia mwenendo wa biashara ya vilainishi na yeyote atakayebainika au kukutwa na vilainishi visivyokidhi ubora atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.



*Mkurugenzi mkuu wa EWURA Dkt. James Andilile*

> “Watumiaji wa vilainishi mnunue vile vilivyosajiliwa na EWURA tu, na muepuke vilainishi vilivyowekwa kwenye chupa zisizokidhi ubora”. Alisisitiza Dkt Andille katika tangazo lake kwa umma.

EWURA inatoa mwito kwa wananchi kuwa makini na bidhaa za vilainishi wanazouziwa na watoe taarifa kwa Mamlaka, mara wanapobaini ukiukwaji wa taratibu, ili kuchukua hatua stahiki. Orodha ya vilainishi vilivyosajiliwa na EWURA ipo kwenye tovuti www.ewura.go.tz





# Fuateni sheria, wadau wa magari ya kutumia gesi asilia waambiwa

**Na. Tobietha Makafu**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imekutana na wadau wenye vituo vya kujaza gesi iliyoshindiliwa (CNG) kwenye magari, karakana za kuweka mifumo ya gesi kwenye magari, waidhinishaji na wakaguzi wa mifumo hiyo na kuwataka kufanyakazi kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo ili kuhakikisha usalama wa huduma,mali, watu na mazingira.

Wadau hao pia wametakiwa kujisajili katika Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa wa Petroli na Gesi Nchini (NPGIS), unaoratibiwa na EWURA ili kuwasilisha taarifa za utendaji wao wa kila siku kwa lengo la kufuatilia mwenendo wa maendeleo ya sekta ya gesi asilia nchini, zitakazoisaidia EWURA kufanya maamuzi ya kiudhibiti na katika kuishauri Serikali.

Hayo yalisemwa na Meneja wa EWURA wa Usambazaji wa Gesi Asilia, Mha. Lucas Nkilila, wakati wa warsha iliyofanyika katika ofisi za EWURA, Kanda ya Mashariki, Dar es Salaam, hivi karibuni.




*Msajili wa Bodi ya Wakandarasi (CRB), Mha. Rhobrn Nkori (Kushoto), Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Bw. Lazaro Msasalaga(Katikati) na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA ambaye pia ni Mkurugenzi wa Gesi Asilia wa EWURA, Mha. Poline Msuya, wakiwa wameshika Hati ya Makubaliano ya Ushrikiano wa Usimamizi wa Shughuli mbalimbali za Gesi Asiilia iliyoshindiliwa (CNG).*

Akifafanua kuhusu mfumo huo, Mha. Nkilila alisema: “Mfumo wa NPGIS, unasimamiwa na EWURA na ulianzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 124 cha Sheria ya Petroli, kwa Dhumuni ya kuratibu taarifa na takwimu zinazohusiana na shughuli za mkondo wa kati na wa chini wa Sekta ya Gesi Asilia na Petroli nchini.”

Baada ya gari kuwekewa mfumo wa gesi asilia iliyokandamizwa, linapaswa kukaguliwa ili kujiridhisha, endapo mfumo huo unakidhi viwango, kisha kuidhinishwa kwaajili ya matumizi na taarifa za ukaguzi huo ni lazima ziwekwe katika mfumo wa NPGIS.

Mha. Nkilila aliwataka wadau hao kutoa maoni na kuuelewa vizuri mfumo, sanjari na kutosita kuwasiliana na EWURA kwa changamoto yoyote watakayokutana nayo wakati wa uwasilishaji wa taarifa katika mfumo wa NPGIS, unaopatikana katika tovuti ya EWURA ya www.ewura.go.tz.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ni miongoni mwa waliohudhuria warsha hiyo, ambapo waliwataka washiriki kuzingatia viwango vya ubora katika kuidhinisha mifumo ya magari yanayorekebishwa na kuwa ya kutumia gesi, kukagua magari hayo, pamoja na kuwa na nyenzo sahihi za kazi.

Kwa upande wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB), walieleza kuhusu utaratibu wa kufuatwa katika usajili karakana za kuweka mifumo ya gesi asilia kwenye magari. Aidha wawakilishi kutoka Chuo kikuu cha Dar es Salaam pia walihudhuria semina hiyo.

# Anachotakiwa muombaji leseni za mafundi umeme nchini sasa ni simu ya Kiganjani

**Na Asiatu Msuya**

Waombaji wa leseni zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) za kufunga mifumo ya umeme nchini, sasa watazipata kupitia simu zao za mkononi ikiwa ni mkakati wa Mamlaka wa kuendelea kurahisisha upatikanaji wa leseni hizo ili kuhakikisha kila fundi umeme nchini anafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Maombi ya leseni hufanyika kieletroni kwa mfumo wa LOIS https://lois.ewura.go.tz/ewura/ kwenye tovuti ya Mamlaka, www.ewura.go.tz na mara baada ya Bodi kuidhinisha leseni hizo, kwa uratatibu wa sasa, mwombaji atapokea kwa simu yake ya mkononi, hivyo kutolazimika kufika ofisini.


Kaimu Mkurugenzi wa Umeme, EWURA, Mha. Erick Rugabera, alisema dhima ya EWURA ni kuhakikisha mafundi umeme wanapata leseni kwa urahisi ili kuwaepusha wateja na majanga yatokanayo na mifumo mibovu ya umeme, isiyozingatia ubora wa kazi na viwango stahiki.

Aidha, ukaguzi wa shughuli za mafundi umeme katika maeneo mbalimbali nchini, umebaini kuendelea kuwapo viashiria vya kazi zilizofanywa na mafundi wasio na leseni, hivyo kutishia usalama wa watu, afya na mazingira.

Ifahamike kuwa, ni LAZIMA kwa fundi umeme kuwa na leseni na kinyume chake hupelekea kutozwa faini, kifungo jela au vyote kwa pamoja.

EWURA itaendelea kuwahamasisha mafundi umeme kuwa na leseni kabla ya kuanza kutoa huduma kwa wateja, ili kupiga vita mafundi vishoka na kuepusha majanga yatokanayo na mifumo hafifu isiyokidhi ubora na viwango. Pia, itaelimisha jamii na wateja kuhusu umuhimu wa kutumia mafundi wenye leseni.



# Kujisajili Kanzidata ya EWURA ni ndani ya saa 24

**Na Asiatu Msuya**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji imeboresha usajili katika Kanzidata ya watoa huduma wa ndani (LSSP) na wataalamu kutoka siku tatu za awali hadi chini ya saa 24, lengo likiwa ni kuhamasisha Watanzania wengi kujisajili kutoa huduma kwenye miradi na kandarasi mbalimbali katika Sekta ndogo ya Petroli na Gesi Asilia.

Usajili wa watoa huduma ni hufanyika bila gharama yoyote kupitia mfumo wa pamoja (CQS) https://cqs.ewura.go.tz/ unaopatikana katika tovuti ya EWURA www.ewura.go.tz. Huduma zinazosajiliwa ni pamoja na bima, usafiri na vifaa, ununuzi, chakula, vinywaji na ukarimu, huduma za afya kutaja chache.

Kampuni za kigeni zinaweza kujisajili kutoa huduma kwa kuingia ubia na kampuni za ndani ambazo lazima ziwe na angalau asilimia 25 ya hisa.

Waombaji wa usajili katika Kanzidata ya LSSP wanatakiwa kuwa na nakala ya cheti cha usajili wa kampuni; nakala ya cheti cha mlipa kodi kilichotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na, nakala ya nambari ya utambulisho wa kodi (TIN).

Nyingine ni nakala ya leseni halali za biashara; nakala ya cheti cha usajili wa kitaaluma kama vile Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania au vyombo vingine vya uthibitishaji;



*Kamishna wa Petroli na Gesi, Bw. Michael Mjinja (katikati) akikata utepe wakati wa uzinduzi wa miongozo ya kulinda miundombinu iliyo chini ya ardhi katika mikuza inayomilikiwa kwa pamoja. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa SONGAS, Dkt. Michael Mngodo (kulia).*

Pia nakala ya hati ya hifadhi ya jamii iliyotolewa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF); barua ya udhamini wa benki / taarifa ya fedha kutoka benki (angalau ya miezi mitatu); taarifa wanahisa kutoka BRELA (kwa wanahisa).

Kwa usajili wa wataalamu, mahitaji ni nakala iliyoidhinishwa ya kitambulisho cha taifa au kadi ya usajili wa mpigakura au pasipoti ya kusafiria; nakala zilizoidhinishwa za sifa za kitaaluma (O-Level, A-Level, Shahada ya Kwanza, Uzamili au PhD); nakala iliyoidhinishwa ya vyeti vya kitaaluma na nakala ya mafunzo ya muda mfupi yaliyofanyika karibuni (chini ya miezi 12) (ikiwa ipo).

Waombaji wa usajili wanaweza kuwasiliana na EWURA kupitia support@ewura.go.tz au kupiga simu bila malipo 0800110030 wakati wa saa za kazi (kuanzia 2:00 asubuhi – saa 10:00 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa).

# Wananchi wahamasishwa kuvuna maji ya mvua

**Na. Tobietha Makafu**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imewahamasisha wananchi wa Dodoma, kuvuna maji ya mvua kutoka kwenye paa za nyumba au yanayotiririka juu ya ardhi kwa kutumia mifumo inayoweza kufungwa majumbani na taasisi ili kukabiliana na uhaba wa maji unaoukabili Jiji la Dodoma.

Uhamasishaji huo umefanyika kupitia madiwani wa kata 67 zilizopo katika Jiji la Dodoma, kwani wana uwezo wa kuelimisha wananchi katika maeneo yao ya kiutawala pamoja na mamlaka ya kutunga sheria ndogondogo ambazo utekelezaji wake utaleta hamasa kwa wananchi kuweka miundombinu ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua.

Akifungua semina hiyo, Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, aliwataka madiwani hao, kutoa hamasa kwa wananchi katika maeneo yao ili waweke mikakati ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua, wakati hatua mbalimbali za kuimarisha huduma ya maji zikiendelea kuchukuliwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) zikifanyika.

Naye Mha. Exaud Fatael, Mkurugenzi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa EWURA, akitoa neno la utangulizi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa EWURA alisema: "Uvunaji wa maji ya mvua ni teknolojia inayohushisha kukusanya na kuhifadhi maji ya mvua kutoka juu ya paa, ardhi na miamba kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile mitungi, matenki, mabwawa na vifaa vingine."



> "Uvunaji wa maji ya mvua ni teknolojia inayohushisha kukusanya na kuhifadhi maji ya mvua kutoka juu ya paa, ardhi na miamba kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile mitungi, matenki, mabwawa na vifaa vingine."

"Utekelezaji wa suala la kuvuna maji ya mvua yanahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali kama Mamlaka za Serikali za Mtaa (LGA), katika kutafuta suluhu ya kuimarisha hali ya huduma ya maji. Aidha Madiwani wanayo nafasi ya kutunga sheria ndogondogo, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wake na kutoa elimu," alisema Mha. Fatael.

Vyanzo vya maji katika Jiji la Dodoma ni visima virefu, ambavyo uzalishaji wake kwa siku ni lita. 67,100,000.00 wakati mahitaji ni lita Mil. 133,844,000.63 kwa siku, Hii inaonyesha kuna upungufu mkubwa wa uzalishaji ukilinganisha na mahitaji, na kufanya wastani wa masaa ya kutoa huduma kuwa 12, hivyo jitihada kubwa zinahitajika kuhamashisha uvunaji wa maji ya mvua," alimalizia Mha. Fatael.

EWURA itaendelea kutoa ushauri kwa Serikali katika kuandaa sera, sheria na kanuni zitakazowezesha kukua kwa sekta ya maji na kuendelea kusimamia watoa huduma ambao ni mamlaka za maji ili kuhakikisha huduma zinakuwa bora kwa manufaa ya wananchi na Taifa.

# Iringa WSSA yawa kinara kwa ubora wa utoaji wa huduma

**By Tobietha Makafu**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) imeibuka kuwa mamlaka bora kwa ujumla katika utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, kati ya mamlaka za mikoa 26, hii ni kwa mujibu wa Ripoti ya Utendaji ya Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2021/22, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Machi 2023.

Kwa upande mwingine, KASHWASA imekuwa ya kwanza kati ya Mamlaka 7 za Majisafi na Usafi wa Mazingira za miradi ya Kitaifa huku Mamlaka ya Maji ya Nzega ikiibuka mamlaka bora katika utoaji wa huduma za maji, kati ya Mamlaka ya Maji 57 za Wilaya na Miji midogo.

Hii ni kwa mujibu wa Ripoti ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2021/22, ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango, katika uzinduzi iliyofanyika mwezi Machi 2023.

Akitoa hotuba ya ufunguzi, Mhe. Dkt. Mpango, ameitaka EWURA, kuendelea kuwafuatilia kwa karibu utendaji wa mamlaka za maji ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Akitoa taarifa ya Ripoti hiyo, Mkurugenzi mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile alisema: Taarifa iliyozinduliwa leo inahusisha uchambuzi wa utendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira 90 ikiwemo; mamlaka 33 za Mikoa na Miradi ya Kitaifa, 51 za miji mikuu ya wilaya na 6 mamlaka za miji midogo".

Aliongeza: "Maeneo yaliyoimarika kwa kiasi kikubwa ni pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Isdor Mpango (katikati) akikata utepe kuzindua Taarifa za Utendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwa mwaka 2021/2022, Machi 2023. Kushoto ni Naibu Waziri wa Maji, Mha. Maryprisca Mahundi na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya. Kulia kabisa ni Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile.*

maji yaliyozalishwa; kupungua kwa kiasi cha maji yanayopotea; kuongezeka kwa kiwango cha ubora wa maji; kuongezeka kwa wateja wa maji na wateja wa mtandao wa uondoaji majitaka; na kuongezeka kwa makusanyo na viwango vya ufanisi katika ukusanyaji maduhuli"

Mamlaka za Maji zilizofanya vizuri katika uwasilishaji wa tozo ya udhibiti ni Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za; Lushoto, Mbinga, Biharamulo, Igunga, Kibaigwa, Kibondo, Kiomboi, Ludewa, Mahenge, Manyoni, Makambako, Mombo, Ngara, Nzega, Orkesumet, Rombo na Tukuyu. Hizi ni mamlaka 17 kati ya 57 za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Makao Makuu ya Wilaya na Miji Midogo na DAWASA, Iringa, Dodoma, Moshi, Mpanda, Njombe and Babati ambazo ni 7 kati ya mamlaka 26 za mikoa.

Mamlaka zilizofanya vizuri katika kudhibiti upotevu wa maji ni MAGANZO miongoni mwa Mamlaka 57 za Makao Makuu ya Wilaya na Miji Midogo. KASHWASA kati ya Mamlaka 7 za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miradi ya Kitaifa. SHINYANGA miongoni mwa Mamlaka 26 za Miji ya Makao Makuu ya Mikoa.

Mamlaka zilizofanya vizuri katika kufikia malengo ya utendaji waliyojiwekea kwenye mipango yao ya biashara ni ORKESUMET kati ya Mamlaka 57 za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Makao Makuu ya Wilaya na Miji Midogo, KASHWASA kati ya mamlaka 7 za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miradi ya Kitaifa na DODOMA kati ya Mamlaka 26 za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji ya Makao Makuu ya Mikoa.

# EWURA kuwasaidia wazalishaji wadogo wa umeme nchini

**Na. Tobietha Makafu**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imekutana na wazalishaji wadogo wa umeme (SPP na VSPP) kujadiliana mambo mbalimbali, zikiwemo changamoto wanazokutana nazo katika utoaji wa huduma ya umeme nchini.



Katika Mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile aliwataka wadau hao kutoa maoni na changamoto zao kwa uwazi, kwa maendeleo ya sekta hiyo ndogo ya umeme.

Baadhi ya wadau waliohudhuria mkutano huo ni pamoja na wawakilishi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Umeme vijijini (REA), Chama cha Maendeleo ya Wazalishaji wadogo wa Umeme Afrika (AMDA) na Chama cha Wazalishaji wa Nishati Jadidifu Tanzania (TAREA).

Wengine ni wawakilishi kutoka kampuni ya Watu na Umeme Ltd, 92 Ltd, Sana group, Masista wa Mbingu, Ludewa Clean Energy, Africa Power, Power Matrix, Power Corner, Power Gen renewable energy, Turiani Hydro, Ngombeni Power Ltd, East Africa Power Ltd, Andoya Hydro Electrical Power na Total Energies. .

Katika mkutano huo, Meneja wa Uchambuzi wa Mahesabu, Bw. Msafiri Mtepa alisema: “EWURA imepokea maoni na changamoto zao, ina ahidi kuzifanyia kazi kwa wakati, ili kuendelea kushamirisha uwekezaji na kulinda mitaji ya watoa huduma sanjari na kulinda maslahi ya walaji”.

kwa mujibu wa sheria ya umeme ya mwaka 2008, EWURA ina jukumu la kusajili wawekezaji wadogo wa umeme chini ya Megawati moja; Kufuta usajili endapo itadhibitika ukiukwaji wa masharti yake na udhibiti ubora wa ufanisi wa utoaji huduma, kwa kutaja machache.